

TANGAZO LA SERIKALI NA. 231 la tarehe 4/4/2025

SHERIA YA UHAMISHAJI WA MAKABURI,
(SURA YA 72)

NOTISI

(Imetolewa chini ya kifungu cha 4(1))

NOTISI YA KUSUDIO LA KUHAMISHA MAKABURI KATIKA ENEO LA KISHENGE
MANISPAA YA BUKOBA YA MWAKA 2025

KWA KUWA, kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria ya Uhamishaji wa Makaburi, Sura ya 72, Waziri mwenye dhamana ya ardhi amepewa mamlaka, endapo atajiridhisha kuwa eneo la ardhi lenye makaburi linahitajika kwa madhumuni ya umma, kuondoa makaburi au maiti katika eneo hilo na kuyahamishia au kuwazika tena katika eneo atakaloidhinisha;

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa kifungu cha 4(1) cha Sheria hiyo kabla ya kuondoa makaburi kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria hiyo Waziri anapaswa kutoa notisi ya kusudio la kuondoa makaburi au maiti katika eneo moja na kuyahamishia au kuwazika tena katika eneo lingine;

NA KWA KUWA, ardhi ya eneo la Kishenge, Manispaa ya Bukoba lenye ukubwa wa hekta 1.89, lenye makaburi 3166 linahitajika kwa madhumuni ya umma ikiwemo matumizi ya biashara na uwekezaji;

HIVYO BASI, Mimi, DEOGRATIUS J. NDEJEMBI, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa mamlaka niliyopewa na, na kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Uhamishaji wa Makaburi, Sura ya 72, natoa Notisi kama ifuatavyo:

*Notisi ya Kusudio la Kuhamisha Makaburi Katika Eneo la Kishenge
Manispaa ya Bukoba*

Tangazo la Serikali Na. 231 (Linaendelea)

- Jina 1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kuhamisha Makaburi katika Eneo la Kishenge Manispaa ya Bukoba ya Mwaka 2025.
- Notisi 2. Notisi inatolewa kwamba Serikali inakusudia kuyaondoa makaburi 3166 yaliyopo katika eneo la Kishenge, Manispaa ya Bukoba lenye ukubwa wa hekta 1.89 na kuyahamishia katika eneo la kiwanja Na. 927 Kitalu "D" Buhembe, Mtaa wa Omukigusha, Kata ya Bilele, Manispaa ya Bukoba kwa mujibu wa masharti ya Sheria baada ya kuisha kwa muda wa siku ishirini na moja tangu tarehe ya kutangazwa kwa Notisi hii.
- Taarifa 3. Taarifa kuhusu makaburi au miili ya marehemu itakayoathirika za zoezi hili zinaweza kukaguliwa katika Ofisi ya Kamishna wa Ardhi, Dodoma, Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Kagera na katika Ofisi ya Afisa Ardhi Mteule wa Manispaa ya Bukoba.
- Haki za ndugu na jamaa wa marehemu 4.-(1) Ndugu wa marehemu waliozikwa katika maeneo hayo anayo haki ya-
- (a) kuwasilisha pingamizi kwa maandishi kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya ardhi dhidi ya hatua inayokusudiwa kuchukuliwa ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu tarehe ya kutangazwa kwa Notisi hii; na
 - (b) kumtaarifu Waziri mwenye dhamana na masuala ya ardhi kwa maandishi kwamba, kwa idhini ya Waziri, atahamisha mwenyewe kaburi husika ndani ya miezi miwili tangu tarehe ya kutangazwa kwa Notisi hii.

(2) Mapingamizi yote au maombi ya idhini ya kuondoa makaburi chini ya aya ndogo ya (1) yawasilishwe kwa Waziri kupitia anwani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,
Mji wa Serikali- Mtumba,
S.L.P 2908,
40477 DODOMA.

Dodoma,
19 Machi, 2025

DEOGRATIUS J. NDEJEMBI
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na
Maendeleo ya Makazi*